



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26 - 2963822
 Nukushi: +255 26 - 296382
 Barua pepe: sg@nbs.go.tz
 Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete
 S. L. P. 2683
Dodoma
TANZANIA



Kumb. Na. BE. 424/455/01/86

Tarehe: 19 Mei, 2022

TAARIFA KWA UMMA WATALII WALIOINGIA NCHINI, KIPINDI CHA JANUARI - APRILI, 2022

Taarifa ya mwenendo wa watalii walioingia nchini ni mionganoni mwa taarifa za muda mfupi (high-frequency data) zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu SURA 351.

Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Januari - April 2022

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Aprili 2022, idadi ya watalii 367,632 kutoka nje ya nchi walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii ikilinganishwa na watalii 275,097 walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2021. Hili ni ongezeko la watalii 92,535 sawa na asilimia 33.6 (**Jedwali Na. 1**). Kati ya watalii 367,632 walioingia nchini, watalii 124,212 waliingia nchini kupitia Zanzibar ambao ni sawa na asilimia 33.8 ya watalii wote.

Watalii walioingia nchini mwezi Aprili 2022, waliongezeka hadi 78,784 kutoka watalii 43,966 walioingia nchini mwezi Aprili 2021. Idadi ya watalii waliongezeka walikuwa 34,818 sawa na asilimia 79.2. Ongezeko hilo limetokana na nchi nyingi duniani kuondoa zuio la kusafiri kufuatia kupungua kwa hali ya maambukizi ya UVIKO-19 na juhudhi za Serikali kuendelea kutangaza vivutio vya utalii nchini.

Jedwali Na. 1: Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Kuanzia Januari Hadi Aprili 2022

	2021	2022	Ongezeko	Badiliko (%)
Januari	79,116	94,128	15,012	19.0
Februari	79,730	100,936	21,206	26.6
Machi	72,285	93,784	21,499	29.7
Aprili	43,966	78,784	34,818	79.2
Jumla	275,097	367,632	92,535	33.6

Chanzo: Idara ya Uhamiaji, 2022

Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Kabla na Baada ya UVIKO-19

Idadi ya watalii walioingia nchini mwaka 2019 walikuwa 1,510,151 ambapo idadi kubwa zaidi ya watalii 160,296 waliingia nchini mwezi Desemba 2019. Baada ya dunia kukumbwa na UVIKO-19, nchi nyingi ziliweka vikwazo vya kusafiri vilivyo sababisha idadi ya watalii walioingia nchini kupungua hadi 620,867 mwaka 2020 ambapo idadi ndogo zaidi ya watalii 7,105 walioingia nchini mwezi Aprili 2020. Mwaka 2021, idadi ya watalii walioingia nchini iliiongezeka hadi 922,692, sawa na asilimia 48.6.

Matarajio ya Idadi ya Watalii Wanaoingia Nchini

Idadi ya watalii wanaotarajiwa kuingia nchini itaongezeka zaidi ya idadi iliyokuwepo kabla ya UVIKO-19 kutokana na juhudi mbalimbali za Serikali za kutangaza vivutio vya utalii ambavyo ni pamoja na mbuga za wanyama, fukwe za bahari, Mlima Kilimanjaro, uwindaji na utalii wa kitamaduni. Aidha, kukamilika na kuanza kurushwa kwa filamu ya *Tanzania, the Royal Tour* iliyozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imeiwezesha *Dunia kuitambua Tanzania*. Kuongezeka kwa viwango vya ukuaji wa shughuli za uchumi zinazohusiana na sekta ya utalii zinazojumuisha Sanaa na Burudani (asilimia 11.7) na Malazi na Huduma za Chakula (asilimia 11.3) ni miongoni mwa viashiria vinavyoonesha kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii nchini.

Kwa mujibu wa Sera ya Mapitio ya Takwimu, takwimu za idadi ya watalii walioingia nchini zinaweza kufanya mapitio endapo takwimu mpya za watalii walioingia nchini zitapatikana kutoka Idara ya Uhamiaji.

*Kwa taarifa zaidi wasiliana na Mtakwimu Mkuu wa Serikali S.L.P 2683 Dodoma,
Simu +255 26 2963822, Nukushi +255 26 296382, Baruapepe: sg@nbs.go.tz, tovuti:
www.nbs.go.tz*